# WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### KUFUNGUA DIRISHA LA MAOMBI YA TUZO ZA UHIFADHI NA UTALII "THE SERENGETI AWARDS" 2025

Napenda kuwajulisha Watanzania wote na wadau wa sekta ya uhifadhi na utalii kwamba dirisha la kupokea maombi ya kushiriki Tuzo za Uhifadhi na Utalii "The Serengeti Awards" 2025 limefunguliwa rasmi kuanzia tarehe 15 Oktoba hadi tarehe 15 Novemba 2025.

Tuzo hizi zimeandaliwa kwa lengo la kutambua, kuheshimu na kusherehekea mchango wa wadau mbalimbali wanaochangia maendeleo ya sekta ya uhifadhi na utalii nchini Tanzania.

Kupitia tuzo hizi, tunalenga kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali, sekta binafsi na jamii katika kulinda rasilimali zetu za asili, kukuza ubora wa huduma, na kuongeza mvuto wa vivutio vya utalii vya Tanzania duniani.

Wadau wote wenye sifa wanakaribishwa kuwasilisha maombi yao kupitia tovuti rasmi ya tuzo hizi: https://www.serengetiawards.go.tz/

Tuzo za mwaka huu zitakuwa jumla ya 56, zikiwa katika makundi makuu saba (7) ambazo ni: People's Choice Awards, Tourism Operator Awards, Tour Guide Awards, Best Accommodation and Restaurant Services, Conservation Awards, Tourism Exhibitor Awards pamoja na Special Appreciation Awards.

Tuzo hizi ni jukwaa la kipekee la kutambua ubunifu, kujituma na ubora wa kazi za wadau wote wa sekta hii muhimu.

Tunaamini kuwa “***The Serengeti Awards***” zitachochea ari ya ushindani chanya, kuboresha huduma, na kuongeza tija katika sekta ya utalii na uhifadhi nchini.

Sherehe ya utoaji wa tuzo inatarajiwa kufanyika tarehe 19 Desemba 2025, ambapo washindi wataheshimiwa kwa mchango wao katika maendeleo ya sekta hii.

Nawakaribisha wadau wote kushiriki kikamilifu katika mchakato huu wa kitaifa wa kutambua ubora.

Kwa maswali, ufafanuzi na maelezo zaidi kuhusu The Serengeti Awards hizi tafadhali wasiliana nasi kupitia namba; 0777-907777 na 0651-212121.

**Balozi Dkt. Pindi H. Chana**
**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII**

**15.10.2025**